USAWA

# DC Taka ataka haki za wanawake

**Asema kuna kesi ni nyingi za wanawake kudai haki zao**

Mussa Juma, Mwananchi
mjuma@mwananchi.co.tz

**Ngorongoro.** Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro Mkoa wa Arusha, Rashid Taka ameshauri kufanyike midahalo kujadili haki za wanawake katika jamii za kifugaji ili kumiliki ardhi.

Akizungumza na Mwananchi kuhusu wanawake kukosa haki ya umiliki wa ardhi katika jamii hiyo, alisema hali hiyo inatokana na mifumo dume, sheria na mila na tamaduni.

Alishauri kuwepo midahalo ya kujadili haki za wanawake kuanzia ngazi za familia, kata na wilaya ili kupata suluhu ya kudumu.

"Kesi ni nyingi za wanawake kudai haki zao, lakini kwanini sisi wanaume tusilizungumze jambo hili hata kabla ya kufariki dunia, hili litasaidia kupunguza tatizo," alisema Taka.

Baadhi ya wanawake katika vijiji vya Arash, Soitsambu, Ngarwa na Loliondo walisema tatizo la kunyimwa haki ya umiliki wa ardhi ni kubwa na jitihada zinahitajika kulitatua.

Mkazi wa Loliondo, Neema Peter alisema suala la umiliki wa ardhi kwa wanawake wa jamii ya kimasai limekuwa changamoto kutokana na uwepo na mila zinazonyima haki ya wanawake.

"Mimipianilikuwanamgogoro wa ardhi baada ya shemeji zangu kutaka kuninyang'anya shamba mume wangu alipofariki dunia, lakini nashukuru nilisaidiwa na viongozi wa Serikali na likaisha lakini bado sina amani," alisema Neema.

Mkurugenzi wa Shirika la Mimutie Women Organization (MWO), Rose Njilo alisema tatizo wanawake wanaolalamika hutengwa.

Alisema katika Kijiji cha Arash wilayani Ngorongoro, Talengo Ole Sayeti ametengwa kutokana na kujitokeza kupambania haki yake ya umiliki wa ardhi.

"Huyu mama amelazwa mara mbili kwa vipigo vya wanaume baada ya kukataa kunyanyaswa kwa kupokonywa ardhi yake,"alisema Njilo.

## Benki ya NBC yachangia saruji kuboresha ujenzi wa shule

Kelvin Matandiko, Mwananchi
kmatandiko@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa mifuko 236 ya saruji kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi 13 katika Manispaa ya Temeke.

Msaada huo unatokana na maombi ya manispaa hiyo ya kuchangia kukarabati na kujenga shule za umma zinazokabiliwa na changamoto hasa uchakavu na ubovu wa miundombinu.

Kaimu mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Deogratius Lukomanya alipokea mifuko hiyo juzi kutoka kwa Mkuu wa huduma za wateja wakubwa wa NBC, Linley Kapya aliyeahidi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali kuboresha elimu, afya, mazingira na maendeleo ya jamii.

**13**
**Idadi ya shule zitakazonufaika na saruji**

Lukomanya alisema shule nyingi katika manispaa hiyo zinapitia marekebisho na ujenzi wa miundombinu hivyo msaada huo utasaidia kukamilisha miradi hiyo.

Mkuu wa huduma za wateja wakubwa wa NBC, Linley Kapya, alisema mifuko hiyo itasaidia kuboresha shule ambazo hazijakamilika.

"Manispaa walitufuata wakiwa na mahitaji haya na tukaona ni muhimu kuunga mkono mpango kama huo, " alisema Kapya.

Alizitaja shule zitakazonufaika katika msaada huo ni shule za msingi Toangoma mifuko 20, Charambe (15), Faraja (10), Mbagala (20), Marten Lumbanga (10), Kibonde Maji (20), Kilimahewa (15), Kingugi (15), Ukombozi (20), Likwati (15), Yombo Dovya (20), Kizuiyani (36) na Nzasa (20).

## UBUNIFU

Mkazi wa Kigoma Tegemeo Dickson akioka moto kwenye jiko rafiki wa mazingira alilolibuni kwa tumia udongo ambalo linatumia kiasi kidogo cha mkaa. Dickson alikutwa akiuza majiko yake Jijini Mwanza jana kwa kati ya Sh80,000 na Sh220,000 kulingana na ukubwa. **Picha na Jesse Mikofu**



## Temeke waanza usafi kuepuka magonjwa

Pamela Chilongola,Mwananchi
pchilongola@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Wila ya Temeke imeanza kufanya usafi katika maeneo mbalimbali ili kuepuka magonjwa ya kipindupindu na kuhara.

Mkuu wa wilaya hiyo, Godwin Gondwe aliwataka wananchi na wafanyabiashara kufanya usafi vinginevyo watachukuliwa hatua za kisheria.

Gondwe alisema wananchi watakaokutwa na uchafu watapewa adhabu papo kwa hapo na Mahakama inayotembea (mobile Court) ikiwamo kulipishwa faini ya Sh50,000.

Mganga mkuu wa wilaya hiyo, Shadrack Shimwela alisema ugonjwa wa Covid-19 umepunguza magonjwa ya kuhara kutokana wananchi kunawa mikono mara kwa mara.

Shimwela alisema kutokana na wananchi wakihofia kupata Covid-19 wamekuwa wakinawa mikono mara kwa mara.

## Barabara ya Ngerengere-Kilunda kujengwa

**"Shirika letu kwa kushirikiana na mkandarasi anayejenga reli tukakubaliana tuanze kuitengeneza barabara hii kwa hatua za awali ikihusisha kuchonga na kushindilia ili vyombo vya usafiri viweze kupata njia ya uhakika ya kupita."**

**Jamila**

Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kushirikiana na kampuni inayojenga reli ya kisasa ya Yapi Merkez imeanza kutengeneza barabara inayounganisha Ngerengere na Kilunda wilayani Morogoro.

Ujenzi huo ni furaja kwa wakazi wa Kijiji cha Matuli ambacho barabara hiyo itapita.

Wakazi hao walisema jana kuwa wamekuwa na adha ya barabara hali kwa muda mrefu hali inayosababisha baadhi kupoteza maisha wakiwa wanafuata huduma za afya katika hospitali iliyopo Ngerengere.

Abdul Mohamed, mkazi wa kijiji hicho alisema barabara hiyo ikitengenezwa itawapunguzia makali ya kutembea umbali mrefu kufuata hospitali kutokana na kukosekana usafiri.

"Hospitali kubwa ipo tarafani Ngerengere kwa mgonjwa kutembelea hadi kule ni mtihani wengi wanafia njiani," alisema Mohamed.

Mkuu wa kitengo cha habari na uhusiano wa TRC Jamila Mbarouk alisema wanashiriki kuitengeneza barabara hiyo kwa sababu ni miongoni mwa maeneo inakopita mradi wa reli ya SGR.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa eneo hilo wameona ipo haja ya kuwajengea wananchi barabara ili kuwapunguzia adha ya usafiri inayowakabili.

"Wakazi wa tarafa hii ndiyo walinzi wa miundombinu yetu ya reli, naweza kusema ni majirani zetu kwa hiyo hata mbunge wao, Hamis Taletale alivyowasilisha ombi lake tukaona tulifanyie kazi," alisema.

Akizungumzia hatua hiyo Taletale ambaye ni mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, alisema anajivunia utajiri mkubwa wa watu alionao na ndiyo atakaowatumia kumsaidia kupeleka maendeleo katika jimbo lake.

"Sina utajiri wa fedha, utajiri wangu ni watu nitaendelea kuzungumza nao watanisaidi kama ambavyo TRC leo wamewezesha baada ya miaka 15 tunashuhudia tinga tinga likichonga barabara hii," alisema.